**FORM A**

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME
# SHULE YA SEKONDARI KIMALA

Shule ya Sekondari Kimala
S. L. P 29
Same
25/04/2024

Mawasiliano :-
Mkuu wa shule-Simu : +255 755979536
Makamu : +255 757872646
Matron: +255719894171
Email : kimalasec@gmail.com
: ismail.ngeya@gmail.com
Kumb Na. KSS/S.1273/OG/07.

---

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………………………………………………………………
S.L.P……………………..
………………………………..

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMALA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2024</u>**

## 1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika **tahasusi** ( mchepuo) wa **HGL, HGLi** kwa mwaka wa masomo **2024/2025** katika shule ya sekondari Kimala. Kwa niaba ya Bodi ya Shule, Walimu. Wafanyakazi na Wanafunzi wa shule hii nakupa pongezi na kukukaribisha kwa moyo wa kindugu hapa shuleni.

Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu mkubwa wa kusoma kwa bidii, kufuata sheria za shule na kushiriki katika shughuli za Ellimu ya kujitegemea. Shule itafunguliwa kwa mhula wa kwanza kuanzia **Tarehe 01/07/2024** na mwisho wa kuripoti ni **Tarehe 15/07/2024**

Shule ya sekondari Kimala ipo **Wilaya ya Same**, Mkoa wa **Kilimanjaro**, Mashariki mwa barabara kuu ya Dar-es-Salaam – Arusha. Shule ipo umbali wa **kilometa 99** toka Same Mjini. Unapofika Same Mjini shuka kituo kikuu cha mabasi. Hapohapo uliza magari yaendayo **Mamba** kituo cha **Mpinji**. Ukifika Mpinji uliza mahali shule ya Sekondari Kimala ilipo, ni umbali wa **kilometa 1** kutoka Mpinji.

Kwa wanaotoka Dar es Salaam kuna basi la moja kwa moja linalokuja hadi Mamba linaitwa **SHETCO** ukifika pakia boda boda kutoka kituoni hadi shuleni nauli ni Tshs **3,000/=**. Kama utashukia Same mjini, panda basi linaloitwa **PHIBA ya Mamba,** nauli kutoka Same mjini hadi Mamba ni Tsh. **10,000/=.**

## 2. MAMBO MUHIMU

### 2.1 SARE ZA SHULE:

- Shati mbili (02) nyeupe mikono mirefu
- Sketi mbili (02) rangi ya DARK BLUE zisizobana -zenye rinda boksi na ziwe **ndefu mpaka chini iguse viatu.**
- Soksi jozi mbili (02) nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi (sio raba)



CamScanner

- Sweta rangi ya dark blue aje nalo (lenye "V" shingoni) – Makoti hayaruhusiwi
- Aje na sketi mbili kijani kibichi rinda box ndefu mpaka chini za **kushindia** (Sketi isiyo ya kitambaa mf. jeans hairuhusiwi)
- Aje na T-shirt mbili rangi ya blue yenye kola na isiwe na **maandishi yoyote** (isiwe light wala darkblue)

**NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi isipokuwa sare ulizoelekezwa hapo juu uje nazo**

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

i. Daftari **06 (4 Quire)** kalamu ya bluu au nyeusi, pensili na rula
ii. Kofa/mkebe (mathematical instrument) kwa wanaosoma Jiografia
iii. Scientific calculator kwa wanaosoma Jiografia
iv. Ream mbili **(02)** ya karatasi-A4 kwa mwaka kwa ajili ya majaribio ya kila wiki na mitihani mingine endelevu
v. English Dictionary (kamusi ya Kiingereza) na Vitabu vya kiingereza (kwa wanaosoma kiingereza)
vi. Kamusi ya Kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma Kiswahili)
vii. Vitabu vya Jiografia (kwa wale wanaosoma Jiografia)
viii. Vitabu vya Historia (kwa wale wanaosoma Historia)
ix. Godoro upana/urefu 3 x 6 unene inchi $2^{1}/_{2}$
x. Shuka mbili (02) rangi ya light blue, mto, foronya na blanket moja (01)
xi. Sanduku la bati kwa usalama wa vifaa vyake.
xii. Taulo,sabuni, mswaki na dawa, rangi ya viatu.
xiii. Sahani, kijiko,bakuli na kikombe vyote vya alluminium.
xiv. Chandarua kimoja (01)
xv. Kanda mbili jozi moja (01)
xvi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xvii. Kwanja 1, jembe 1,hard broom 1, mfagio 1 wa nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

### 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;



CamScanner

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;



CS CamScanner

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**5. Uje na:-**

- vyeti halisi (original) na vivuli vyake kama ifuatavyo:
- Result slip
- Cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
- Cheti cha kuhitimu kidato cha Nne (leaving Certificate)
- Passport size (02) yenye blue kwa nyuma na uwe umevaa shati la shule.
- Folder file mbili (02)-rangi ya khaki

**AKAUNTI ZA SHULE:**

- MALIPO YAWEKWE KATIKA **AKAUNTI YA SHULE YA SEKONDARI KIMALA NAMBA 40510004656 (NMB)-Kimalasec school development A/C**

**Kisha ulete risiti (Pay In slip) kutoka benki uliyolipia malipo hayo ya shule. HATUPOKEI FEDHA TASLIMU**

**<u>VIFAA VYA MICHEZO:</u>**

- Raba jozi moja (01)
- Aje na truck suit isiyo na maandishi (koti na suruali yake) rangi ya blue

***KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMALA.***

**ISMAIL T. NGEYA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULEYA SEKONDARI KIMALA
S.L.P 29
SAME



CamScanner

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule : 0755979536
- Makamu Mkuu wa Shule : 0757872646
- Mwandamizi Taaluma : 0659607349
- Mwandamizi Malezi :0625958475



CamScanner

**FOMU B**

MGANGA MKUU,

……………………………………..

……………………………………..

YAH: **UCHUNGUZI WA AFYA YA MWANAFUNZI.**

Mwanafunzi ………………………………………………………………. amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika Shule ya sekondari Kimala. Kabla ya kujiunga katika shule hii na kuendelea na masomo ni lazima apimwe afya yake kama inamruhusu kuendelea na masomo ya kidato cha tano. Tunaomba umfanyie uchunguzi.(Medical examination).

| NA. | MAGONJWA | NDIYO (V) | HAPANA (X) |
|---|---|---|---|
| 01 | Masikio | | |
| 02 | Macho | | |
| 03 | Kifafa | | |
| 04 | Moyo (heart disease) | | |
| 05 | Magonjwa ya akili (Mental illness) | | |
| 06 | Ukosefu wa damu (Anemia sickle cells) | | |
| 07 | Kifua kikuu (T.B) | | |
| 08 | Pumu (Asthmatic case) | | |
| 09 | Kisukari | | |
| 10 | Vidonda vya tumbo | | |
| 11 | Kichocho (Bilharzias) | | |
| 12 | Magonjwa ya zinaa (sexual Transmitted Diseases) | | |
| 13 | Mimba | | |

Je ana dosari nyingine kiafya/ Ugonjwa mwingine (Eleza)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

**MAELEZO YA DAKTARI:** Baada ya uchunguzi. Nimeona/ sikuona dosari yoyote katika afya ya mwanafunzi huyu. Ametibiwa/ Hakutibiwa/ Hastahili/ Anastahili kuendelea na masomo (kataisiyohusika)

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

______________________________

**MGANGA MKUU**

**SAHIHI NA MHURI WA OFISI**



CamScanner

## 1. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi:………………………………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa:..……………………………………………………………………………

Uraia Mtanzania / Sio Mtanzania:……………………………………………………………………

Shule ya sekondari aliyotoka:……………………………………………………………………...

Jina la mzazi/mlezi:……………………………………………………………………………….

Anwani ya mzazi/mlezi:…………………………………………………………………….…

Kitongoji /kijiji anapoishi mzazi/mlezi:……………………………………………………………...

Namba za simu za mzazi/mlezi:……………………………………………………………......

Kazi ya mzazi / mlezi:………………………………………………………………………

## 2. MKATABA WA KUZINGATIA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi …………………………………………………..(jina la mwanafunzi) nakiri kuwa nimesoma na kuelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Kimala. Naahidi kuzingatia na kwamba nikienda kinyume na maelekezo hayo niadhibiwe na kufukuzwa shule itakapokuwa imelazimu.

**Tarehe:……………………….……Sahihi:……………………………………**

## FOMU C-MZAZI/MLEZI

Mimi ………………………………………………………………….…….ambaye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………(jina la mwanafunzi) nimesoma maelekezo na maagizo kwa mwanafunzi na ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika kumlea kijana katika mwenendo na maadili mema. Aidha naahidi kutimiza mahitaji yake yote kwa wakati ili kuepuka kumkwamisha mwanafunzi katika swala zima la taaluma.

**Tarehe:……………………………** **Sahihi mzazi/mlezi:……………………………**



CS CamScanner